# Mwenge wa Hadithi Fupi

## Misingi na Nadharia



Fred. C. N. W. Simiyu
Ernest Sangai Mohochi
Leonard Leo Sanja

# Mwenge wa Hadithi Fupi: Misingi na Nadharia

Kimetolewa zawadi kwa Maktaba ya Chuo Kikuu cha Kibabii (Kona ya Ken Walibora) na Mwandishi.

01/07/2026

Fred. C. N. W. Simiyu
Ernest Sangai Mohochi
Leonard Leo Sanja

© Simiyu, F. C. N. W., Mohochi, E. S., na Sanja, L. L., 2026.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupigisha chapa, kutafsiri au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini, kwa maandishi ya waandishi.

Chapa ya kwanza 2026

**ISBN 978-9966-59-028-2**

Kimechapishwa na:
Tunu Publishers Limited
Barabara ya Savannah
Donholm Shopping Center
Nairobi
Simu: +254 722 682 129/+254 795 689 523
Baruapepe: tunupublishers@gmail.com

# Dibaji

Kuna mwafaka wa kiujumla kuwa, utanzu wa Hadithi Fupi umekua na kupanuka sana katika miaka ya hivi karibuni, haswa kutokana na kuidhinishwa kwênye mitaala ya masomo nchini Kenya na ukanda wa Afrika Mashariki. Hata hivyo, kuna maswali mengi ya kitaaluma ambayo yamekuwa yakiibuka mara kwa mara. Baadhi ya hayo masuala ni kama: Utanzu huu ufasiliwe na kuainishwa kama kipera cha fasihi simulizi ama cha fasihi andishi? Je, ufupi wa hadithi fupi ni idadi ya maneno, uchache wa kurasa ama ni dhana ya kisimulizi tu? Wahusika wa hadithi fupi wawe wangapi na je, mwandishi anaweza akasimulia mawanda mapana badala ya kujibana kwenye suala moja pekee katika maisha ya mhusika mkuu? Mandhari yanaweza kupanuliwa nje ya mipaka ya kauli ya Poe? Je, hadithi fupi inaweza kusimulia na kuibua masuala mazito na ya kina ambayo yanaweza kudhihirishwa kinadharia kama vile riwaya bila kutatanika iwapo haikusomwa kwenye kikao kimoja? Je, hadithi fupi ni muhtasari wa riwaya ama ni utanzu ambao unaweza kujitegemea kinadharia?

Baadhi ya wataalamu hata wamepiga hatua kwa kusema kuwa, hadithi fupi ina msingi wake katika vipera vya fasihi simulizi. Kwa hivyo basi, huu si utanzu mgeni na unaweza kuainishwa katika fasihi simulizi, hivyo kuufanya utanzu unaoyumba kiufasili na kiuainishaji. Hicho ndicho kinaibua mjadala wa iwapo hadithi fupi ni utanzu wa fasihi simulizi ama fasihi andishi. Hata hivyo, uainishaji wa fasihi simulizi wenyewe pia una matatizo maana wanaojaribu kuainisha vipera vya fasihi simulizi haswa vya hadithi, hawajakubaliana kuhusu idadi na vigezo vya uainishaji. Kutobainika huko ndiko kumetoa motisha kwa uandishi wa kitabu hiki: *Mwenge wa Hadithi Fupi: Misingi na Nadharia.* Kitabu hiki ni moja kati ya juhudi za kujaribu kuliziba hilo pengo la uainishaji na ufasili kuhusu utanzu wa hadithi fupi. Kinatilia maanani dhana kwamba, kuibua mijadala na kutokubaliana katika masuala ya kiusomi ndicho kichocheo kikubwa ambacho huongoza juhudi za kiusomi na kuchochea tafiti mpya. Kwa lengo hilo, kitabu hiki kimezingatia nadharia mbalimbali za awali na mpya, ambazo ni muhimu katika kuzamia ufasili, uainishaji na hatua za kina za kutathmini hadithi fupi katika fasihi ya Kiswahili.

Kitaaluma, fasihi andishi imegawika katika tanzu kama riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi. Hata hivyo, kutokana na kukua kwa teknolojia na mawanda ya

kiusomi, kuna tanzu ibuka kama vile wasifu na otografia pamoja na Fasihi Pepe (*Digital Literature*) au Sanaa Pepe (*Virtual arts*) ambayo imeshika kasi miaka ya karibuni. Kwa kuwa fasihi yote ni sanaa inayohusu maisha ya binadamu, suala la kuangazia na kuifafanua kikamilifu kinadharia linakuwa muhimu. Hadithi fupi umekuwa utanzu maarufu kwa kuzungumzia mifumo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kiteknolojia, kimazingira na tabianchi pamoja na hali za kitamaduni za jamii mbalimbali. Kinachobainika kutokana na namna waandishi wanavyobuni masuala haya ni kuwa, utanzu wa hadithi fupi kama vile tanzu nyingine za fasihi, una historia ndefu, una kina kirefu na unajitosheleza kama utanzu. Suala la uainishaji na ufasili wake haliwezi kuunyima utanzu huu haki ya kuchanganuliwa kinadharia kama tanzu nyinginezo.

# Shukrani

Kitabu hiki kimeandaliwa kwa miaka mingi pamoja na kuchangiwa na wataalam mbalimbali, haswa wanafunzi wetu. Kwa hivyo basi, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wanachuo mbalimbali waliochangia maandalizi ya kitabu hiki kupitia mijadala yetu ya darasani, kazi mradi na utafiti wa masuala kadha wa kadha. Kwa hakika, sehemu nyingi za kitabu hiki ni matokeo ya mijadala yetu katika madarasa ya wazamilifu. Baadhi ya hawa wanafunzi wetu ni pamoja na Noah Munda Majele, Fred Wanjala Wanyonyi, Paul Wasike, Christine Nekesa Nyongesa, Nester Ateya, Jenniffer Chepleting Koech, Maurine Mwaniga, Paul Andrew Shikanda, Melvin Atieno Ouma, Victor Gachunga Gatimu, Winnie Musailo Wekesa, Peris Mwihaki, Hillary Mauka Mukoya, Morris Waswa na Neemor Nanjala Wanjala. Naomba wengine wote ambao hatukuwaja wapokee shukrani zetu. Tunatarajia kuwa, kitabu hiki kitakuwa kichocheo cha kuibua hamasa ndani ya waandishi, wasomaji na wahakiki wa fasihi na haswa katika utanzu wa hadithi fupi. Tuna imani kwamba, wazo la kutetea, kuinua na kuimarisha utanzu wa hadithi fupi limejadiliwa vyema kupitia sura mbalimbali za kitabu hiki. Ni matumaini yetu kuwa, *Mwenge wa Hadithi Fupi: Misingi na Nadharia* kitatoa mwangaza angavu kuhusu taaluma hii ya hadithi fupi. **(Waandishi, Juni 2026).**

# Yaliyomo

**Dibaji** .................................................. iii

**Shukrani** .................................................. v

**Utangulizi** .................................................. xi

**Misingi ya Hadithi Fupi** .................................................. 1

Utangulizi .................................................. 1

Misingi ya Hadithi Fupi ni Gani? .................................................. 1

Dhana ya Hadithi Fupi .................................................. 4

Hadithi Fupi ni nini haswa? .................................................. 5

Muhtasari .................................................. 8

Sifa za Hadithi Fupi .................................................. 9

Ufaafu na Umaarufu wa Hadithi Fupi .................................................. 14

Maoni Kuhusu Uandishi wa Hadithi Fupi .................................................. 17

Kupuuzwa kwa hadithi fupi .................................................. 21

Hitimisho .................................................. 30

**Historia na Maendeleo ya Hadithi Fupi** .................................................. 31

Utangulizi .................................................. 31

Hadithi Fupi Uliwenguni .................................................. 31

Dhana ya Bunilizi .................................................. 31

Mikabala ya Bunilizi .................................................. 33

Nadharia ya Bunilizi Etiolojia .................................................. 35

Uwasilishaji wa Hadithi na Mpito wa Wakati .................................................. 38

Hadithi Fupi Katika Maandishi .................................................. 39

Athari ya Ngano Katika Hadithi za Kubuni .................................................. 43

Hadithi Fupi Barani Afrika .................................................. 48

Hitimisho .................................................. 50

**Hadithi Fupi ya Kiswahili** .................................................. 51

Utangulizi .................................................. 51

Historia ya Hadithi Fupi ya Kiswahili .................................................. 51

Nafasi ya Magazeti Katika Ukuzaji na Uendelezaji wa Hadithi Fupi Ughaibuni ... 56

Afrika Mashariki ....58
Nafasi ya Redio Katika Ukuzaji na Uendelezaji wa Hadithi Fupi ....59
Nafasi ya Akili-Unde Katika Ukuzaji na Uendelezaji wa Hadithi Fupi ....60
Dhana ya Sanaa Pepe (*Virtual Arts*) ....61
Sifa za Sanaa Pepe ....62
Nadharia ya Wingi-Mifumo (*Multimodal Theory*) Katika Sanaa Pepe ....65
Sanaa Pepe Kama Zana ya Uwasilishaji wa Hadithi Fupi ....67
Changamoto za Akili-Unde katika Fasihi Pepe ....71
Hitimisho ....72
**Hadithi Fupi katika Mjadala wa Fasihi Linganishi ....73**
Utangulizi ....73
Dhana ya Fasihi Linganishi ....73
Mkururo wa Kifaransa ....74
Mkururo wa Kimarekani ....79
Mkururo wa Kijerumani ....81
Mkururo wa Kilimwengu ....83
Hitimisho ....84
**Fani na Maudhui katika Hadithi Fupi ....85**
Utangulizi ....85
Dhana ya Fani ....85
Dhana ya Maudhui ....96
Maudhui katika Tumbo Lisiloshiba ....111
Muhtasari wa hadithi ya *Nizikeni Papa Hapa* ....112
Kusawiriwa kwa kifo katika *Nizikeni Papa Hapa* ....114
Hitimisho ....114
**Hadithi Fupi kwa Mtazamo wa Wasifu na Otografia ....115**
Utangulizi ....115
Fasihi ya Kihistoria ....115
Kumbukumbu za Utamaduni ....116
Kanuni za Fasihi ya Kihistoria ....117
Wasifu na Otografia ....120

Dhana ya Wasifu ....................................................................................................120
Dhana ya Otografia ...............................................................................................120
Uhusiano wa wasifu na otografia ........................................................................121
Kumbukumbu (*Memoir*) na Kumbukizi (*Memory*) .................................................122
Masimulizi na maandishi yā wasafiri kama otografia ..........................................123
Sifa za Wasifu na Otografia ..................................................................................125
Otografia Shirikishi ...............................................................................................126
Hitimisho ...............................................................................................................142
**Nadharia za Ubunaji wa Fasihi ...........................................................................143**
Utangulizi .............................................................................................................143
Waandishi wanatumiaje Nadharia za Ubunaji? .....................................................143
Nadharia ya Taratibu za Usimuliaji (*Oral Formulaic Theory*) ..............................146
Nadharia ya Utendaji (*Performance Theory*) .........................................................149
Nadharia ya Wingi-Mifumo (*Multi-modal Theory*) .................................................151
Nadharia ya Uunganishaji (*Convergence Theory*) ..................................................154
Nadharia ya Hisia (*Emotionalism Theory*) ............................................................156
Nadharia ya Uamilifu-Ala (*Instrumentalism Theory*) ............................................158
Nadharia ya Utatu (*Third Space Theory*) ...............................................................159
Nadharia ya Skima (*Schema Theory*) ....................................................................164
Hitimisho ...............................................................................................................165
**Nadharia za Uhakiki wa Fasihi ...........................................................................167**
Utangulizi .............................................................................................................167
Dhana ya Nadharia ...............................................................................................167
Nadharia ya Uhistoria Mpya .................................................................................173
Nadharia ya Usemezano .......................................................................................177
Nadharia ya Uhakiki Mazingira ............................................................................180
Mkabala wa Ufeministi-Mazingira ........................................................................182
Mkabala wa Fasihi Mazingira Kimaeneo ..............................................................183
Nadharia ya Ujitambulishaji (*Social Identity Theory*) ............................................184
Nadharia ya Ujumi wa Kiafrika ............................................................................189
Nadharia ya Mwingilianomatini ...........................................................................191


Nadharia ya Vikale (*Archetype Theory*) ..... 194
Nadharia ya Kanivali (*Canivalism Theory*) ..... 198
Nadharia ya Uhusanishaji (*Hermeneutics Theory*) ..... 212
Hamenitiki ya Sasa ..... 214
Nadharia ya Uwazimu ya Hegel (*Hegel's Theory of Madness*) ..... 216
Hitimisho ..... 224
**Uhakiki wa Hadithi Fupi Kinadharia ..... 225**
Utangulizi ..... 225
Muhtasari wa Mzimu wa Kipwerere ..... 226
Uchambuzi wa Mzimu wa Kipwerere ..... 228
Dhana ya Umahuluti wa Kitamaduni ..... 230
Mihimili ya Umahuluti wa Kitamaduni ..... 231
Muhutasari wa Hadithi Fupi ya *Damu Nyeusi* ..... 231
Uchambuzi wa *Damu Nyeusi* ..... 232
Dhana ya Uchawi ..... 234
Uhakiki kulingana na Mtazamo wa Afrosentriki ..... 242
Uafrosentriki katika *Damu Nyeusi* ..... 245
Udadisi wa Kielimu (*Epistemic Curiosity*) ..... 252
Muhtasari wa hadithi ya *Fadhila za punda* na *Nipe Nafasi* ..... 253
Muundo wa Kimaana wa Hadithi za *Fadhila za Punda na Sabina* ..... 265
Muundo wa Ishara na Urejeleo Katika *Fadhila za Punda na Sabina* ..... 268
Muundo wa Migongano ya Kimaana katika *Fadhila za Punda na Sabina* ..... 270
Uhusiano wa Lugha na Maana katika *Fadhila za Punda na Sabina* ..... 271
Muundo wa ujumbe katika Fadhila za Punda na Sabina ..... 272
Hitimisho ..... 273
**Marejeleo ..... 275**

… Kuna idadi kubwa sana ya hadithi ambazo huachwa nje katika ufafanuzi kutokana na ufinyu ambao nadharia ilivyo kijadi, imefanya zitupiliwe mbali na wahakiki, wasomi na wachapishaji (Carpenter na Neumeyer, 1974; Allen, 1981; Tindyebwa, 1988; Shaw 1983; De Grandsaigne, 1985 na Kibera, 1988). Hii ndio maana waandishi wa *Mwenge wa Hadithi Fupi: Misingi na Nadharia* wanabainisha uhusiano wa hadithi fupi na taaluma ya fasihi linganishi; pamoja na utokeaji wa hadithi fupi kama wasifu au otografia. Fauka ya hayo, Simiyu na wenzake wamepanua uwanda wa nadharia za ubunaji pamoja na za uhakiki wa fasihi. Maoni ni kwamba, watunzi huzingatia au huelekezwa na nadharia za utunzi, wakati mwingine bila kujua. Wahakiki nao hufanya kazi yao kwa kuongozwa na nadharia za uhakiki wa fasihi … Isitoshe, mawazo ya waandishi kupitia wahakiki ndio huongoza maarifa ya kiusomi na ndiposa kuna maelezo kuhusu nadharia ambazo hazijatumika kwa mapana katika fasihi ya Kiswahili katika kitabu hiki. Natagemea kitabu hiki kitatoa mwamko mpya wa kuwazia jinsi ambavyo utanzu huu umekuwa ukihakikiwa na hata kuwafaa waandishi hatimaye kubadilisha mitazamo na kunoa kalamu zao hata zaidi.


Prof. R. M. Wafula, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Juni 2026.



**Fred, C. N. W. Simiyu** ni msomi, mwalimu na mwandishi wa Fasihi, Tafsiri, Utamaduni na Lugha ya Kiswahili mwenye tajriba pana. Kufikia sasa, Simiyu ameandika hadhithi fupi tatu: *Kisima chenye Hekima, Nizikeni Mtandaoni* na *Ulumbi wa Ipara*. Kadhalika, amehariri diwani ya *Kisima chenye Hekima na Hadithi Nyingine* pamoja na *Ulumbi wa Ipara na Hadithi Nyingine*. Isitoshe, yeye ndiye Mhariri Mkuu wa TAALUMA, Jarida la CHAKITA. Aidha, Simiyu ndiye mwandishi wa *Kitovu cha Fasihi Simulizi; Misingi ya Ukalimani na Tafsiri; Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili; Concice Trilingual English-Kiswahili-French Dictionary; Safina ya Utafiti wa Fasihi Simulizi;* na *Kiswahili na Uchumi wa Kidijitali*. Kwa sasa, yeye ni Mwenyekiti wa CHAKITA na Mhadhiri Mwandamizi wa Taaluma za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii, Bungoma - Kenya; na Mtafiti wa Lugha za Kiafrika katika *the University of the Free State*, South Africa.



**Ernest Sangai Mohochi** ni Profesa wa Taaluma za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii ambapo anahudumu pia kama Mkurugenzi wa Kituo cha Taaluma za Lugha na Utamaduni (KITALU). Mohochi amefundisha kozi mbalimbali za isimu na fasihi ya Kiswahili kwa zaidi ya miaka thelathini katika vyuo vikuu sita tofauti ndani na nje ya nchi ya Kenya. Miongoni mwa kozi alizozifundisha ni kozi ya Hadithi Fupi ya Kiswahili. Katika upande wa fasihi, Mohochi amebobea zaidi katika utanzu wa hadithi fupi. Sangai amechapisha hadithi fupi nne kufikia sasa: *Ufunguo, Nilimwamini Baba, Uchachu Huja Baadaye* na *Kadhia za Maandamano*. Aidha, Mohochi ameandika makala nne kuhusu hadithi fupi katika majarida mbalimbali.



**Sanja Leo Leonard** ni mwandishi na mhariri tajika wa hadithi fupi. Ndiye mhariri wa diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi nyingine, Alionja Asali na Hadithi Nyingine* na *Kisima chenye Hekima na Hadithi Nyingine*. Sanja ndiye mwandishi wa hadithi fupi tano: *Mimba Ingali Mimba, Kasalia, Kwekwe la Utumwa, Ndoto ya Pacha na Pachika* na *Sumu ya Neno*. Kwa sasa, Sanja ni Mhadhiri wa Fasihi na Lugha katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

ISBN 978-9966-59-028-2

9 789966 590282

Tunu Publishers Limited
Barabara ya Savannah
Donholm Shopping Center, Nairobi
Simu: +254 722 682 129/+254 795 689 523
Baruapepe: tunupublishers@gmail.com